



vi) Kiatu cha baba kimepotea. Neno lililopigiwa mstari ni; ( )

- A. Kivumishi cha kuonesha      B. Kivumishi cha pekee  
C. Kivumishi cha A – unganifu      D. Kivumishi cha jina kwa jina

vii) Mjomba "alikuwa" mgonjwa .Neno lililopigiwa mstari ni :

- A. kitenzi kisaidizi      B. kitenzi kishirikishi  
C. kitenzi kikuu      D. Kitenzi kikurupushi

viii) Kusoma kwake kwa bidii kumempatia mafanikio neno lililopigiwa mstari ni:

- A. kitenzi      B. kitenzi kikuu      C. kitenzi jina      D. kitenzi kisaidizi ( )

ix) Watano wametoroka , neno lililopigiwa mstari ni

- A. kielezi cha idadi      B. kivumishi cha idadi      C. kiwakilishi cha idadi ( )  
D. Nomino ya ujumla

x) Tuimbe sote, ni ;

- A. Wingi nafsi ya kwanza      B. wingi nafsi ya pili      C. Umoja nafsi ya kwanza  
D. Umoja nafsi ya pili ( )

2. Tafakari kwa makini orodha A na B, kasha eleza maana ya vifungu vya maneno katika orodha A kwa kutumia orodha B. (alama 5)

<u>ORODHA A</u>	<u>ORODHA B</u>
i. Tungo tata ii. Kosa la mpangilio mbaya wa viambishi iii. Rejesta ya vijiwani iv. Makosa ya upatanisho wa kisarufi v. Tungo shurutia	A. Mtoto amedondoka chini B. Mwalimu amefundisha vizuri C. Anampigia pasi D. Juma anasoma na anaandika E. Mpe gari F. Ng'ombe zangu wanatoa maziwa mengi G. Angeliniita ningetika H. Mshikaji leo noma he I. Ukiniona ndani ya basi nitakulipia nauli

MAJIBU

<u>ORODHA A</u>	<u>i</u>	<u>ii</u>	<u>iii</u>	<u>iv</u>	<u>v</u>
<u>ORODHA B</u>					

**SEHEMU B (ALAMA 40)**

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii

3. Eleza matumizi ya neno kwa katika sentensi zifuatazo:

- a. Walikusanyika wazee kwa vijana
- b. Nimekuja kwa mguu
- c. Amekuja kwa wito wako
- d. Mgonjwa amekula kwa shida

4.a) misimu ni nini?

b) Eleza chanzo cha misimu (angalau vyanzo vitatu)

5. Istilahi moja inaweza kuwa na majina mawili. Andika majina mengine ya dhana zifuatazo;

- |                |                      |
|----------------|----------------------|
| i. Chagizo     | iii. Prediketa       |
| ii. Shamirisho | iv. Mofimu za wakati |

6. Toa mifano ya sentensi katika kila ngeli zifuatazo;

- |              |           |
|--------------|-----------|
| a) YU/A – WA | e) I – Zi |
| b) U – I     | f) U – Ya |
| c) Li – Ya   | g) KU     |
| d) Ki – Vi   |           |

7. Kwa kutumia hoja sita (6) eleza mambo yaliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.

8. Wewe Shamimu Tawakal umeajiriwa katika Hoteli kama Ofisa manunuzi. Hoteli yako inakabiliwa na upungufu wa vyombo vifuatavyo; vijiko dazeni kumi, bakuli dazeni kumi, sahani dazeni kumi na tano, vikombe dazeni kumi na tatu na bilauri dazeni nane.

Onyesha mfano wa barua ambayo utamwandikia ofisa mauzo wa kiwanda cha vyombo vya ndani Ndugu Mwambe Nkwalulo ili kuagiza vyombo hivyo. Anwani yako ni Mzalendo Hotel S.L.P 2020, Ipole. Jina la kiwanda ni kiwanda cha vyombo vya ndani na anwani yake ni S.L.P 15 Mpanda. Tarehe ni 20/09/2019.

### **SEHEMU C (ALAMA 45). FASIHI KWA UJUMLA**

Jibu maswali matatu tu katika sehemu hii.

9. “Kazi ya fasihi ni kupiga vita mambo yanayokwamisha maendeleo ya jamii” Jadili kauli hii ukionesha jinsi waandishi wawili wa diwani ulizosoma walivyotekeleza hili kwa kutoa hoja tatu kutoka kila diwani.

10. a) Visa asili ni nini?

b) Tunga kisa asili kimoja kuhusu “Mnyama unayempenda”

11. Uongozi mbaya ni sumu ya maendeleo ya familia na Taifa kwa ujumla. Jadili kauli hii ukitumia mifano ya vitabu viwili ulivyosoma (Riwaya). Toa hoja tatu kwa kila riwaya.

12. Malezi ya watoto imekuwa ni changamoto kubwa katika jamii. Jadili sababu tatu (3) kwa kila tamthiliya mbili ulizosoma.

ORODHA YA VITABU

**RIWAYA**

Takadini – Ben J. Hanson (MBS)

Watoto wa mama ntilie – E.Mbogo (H.P)

Joka la Mdimu - A.J. Safari (H.P)

**USHAIRI**

Wasaktonge – M.S Khatibu (DUP)

Malenga Wapya – TAKILUKI (DUP)

Mashairi ya Chekacheka – T.A Mvungi (EP &D. LTD)

**TAMTHILIYA**

Orodha – Steve Reynolds (MA)

Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe – E. Semzaba (ESC)

Kilio Chetu – Medical Aid Foundation (TPH)